# MALEZI YA VIJANA

# NA

# SAFARI YA NDOA BORA

Na Mwl. Pancrasia Paul

"Mtafute Anayekutafuta"

Toleo la 2
Feb 2023

Simu:+255 752 883 265
+255784 264 301
Email: inchargetz@gmail.com
Insta: incharge_tz
website: incharge.co.tz
ISBN 978-9912-40-45-458-8

*Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili,kudurufu au kutumia kitabu au sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na mchapaji. na ukiukwaji wa taratibu hii inaweza kupelekea mashitaka toka kwa waandaaji wa kazi hii.*

**Kimesanifiwa (Designer) na**
**Ayubu D. Laurian Simu: 0748 305 015/ 0620 804 200 Insta: Ivantanzania**

**Kimechapwa na Moccony printing press**
**Dar es Salaam-Tanzania**
**Barua pepe: Mocconyprinting@gmail.com**
**Simu: 0718 908 631 / 0754 857 943**

Na kichapwe (Imprimatur)

Pd. Dkt. Joseph Peter Mosha

Mratibu wa Idara ya Teolojia

Jimbo Kuu la Dar-es-Salaam

01 Novemba 2022

# YALIYOMO:

Utangulizi vi
Dibaji ix
Malengo xii
Shukrani xiii
Pongezi xvi

**Sura Ya Kwanza**
1.0 Malezi ya Vijana 1

**Sura Ya Pili**
2.0 Kwa nini Kijana na Safari ya NDOA Bora? 7
2.1 Safari ya Ndoa Bora 9
2.2 Kwa nini Maandalizi ya Ndoa?
Tena ya muda mrefu? 10
2.3 Safari ya Ndoa Bora Inaanzia wapi? 14

**Sura Ya Tatu**
3.0 Sifa Za Kijana Anayefaa Kuanza
Maisha Ya Ndoa 17
3.1 Ni Umri Upi Mzuri Na Muafaka Wa Kijana
Kuoa au Kuolewa?. 18
3.2 Namna Ya Kumtafuta Rafiki Anayefaa Kwa
Ndoa Bora (Mtafute Anayekutafuta) 20
3.3 Vipengele Muhimu Katika Kufahamiana/
Kuchunguzana; 24

**Sura Ya Nne**
4.0 Mambo Yanayotakiwa Katika Hatua Ya
Urafiki, Hatua Ya Kufahamiana (The Do's) 40

4.1 Mambo yasiyotakiwa katika hatua ya Kufahamiana (The Dont's) 42
4.2 Nitamtambuaje Wa Kufanana Nae? Nitampata wapi? 47

**Sura ya Tano**
5.0 Kijana na Tafakari binafsi baada ya hatua Ya Uchunguzi Kukamilika. 50

**Sura Ya Sita**
6.0 Hatua ya Uchumba 54
6.1 Yanayotakiwa kufanyika katika hatua ya Uchumba 56
6.2 Yasiyotakiwa kufanyika katika hatua ya Uchumba 57

**Sura Ya Saba**
7.0 Mitazamo ya vijana wa sasa juu ya maisha ya ndoa na changamoto zake. 59
7.1 Ushauri kwa vijana wanaotamani kuishi maisha ya Ndoa Bora ya Kudumu 65

**7.2 Hitimisho 69**
Marejeo/bibliografia 70

# UTANGULIZI

**Ulimwengu** wa sasa umegubikwa na wimbi kubwa la majanga. Moja ya majanga ambayo yamekithiri ni hali ya familia kukosa ***utulivu wa fikra.*** Hii inatokana na waasisi wa familia (Wanandoa) kushindwa ***kusimama katika nafasi zao,*** kushindwa kujiweka sawa na pia kushindwa kuishi maisha halisi ya Ndoa. Hali hii pia inatokana na wanandoa kushindwa kutimiza wajibu wao wenyewe kwa wenyewe, kwa watoto wao na kwa wanafamilia wengine wakiwemo ndugu wanaoishi nao katika familia. Ni dhahiri kwamba waasisi wa familia (Wanandoa/Baba na Mama) ndio wenye mamlaka ya kuamua waishi maisha ya ndoa ya namna gani, walee watoto wa namna gani, waishije na ndugu walioamua kuishi nao katika familia zao na mengine mengi katika familia.

Changamoto kubwa ya malezi inatokana na waasisi wa familia (Wanandoa) kukosa muda wa kukaa na watoto wao na kuwasikiliza. Waasisi wa familia wanashindwa kufanya kazi yao ya walimu wa kwanza, kwamba malezi asilia ya mtoto yanatoka kwa wazazi ambao ndio ***walimu wa kwanza*** wa mtoto.

Inapotokea wazazi wanashindwa ***kusimama katika nafasi zao*** kama wazazi, inasababisha malezi ya watoto kuwa dhaifu na kusababisha Taifa lenye watoto wengi wa mitaani. Taifa lenye watoto wengi wanaolelewa na mabibi na mababu, wanaolelewa na mzazi mmoja ambapo malezi yao kwa asilimia kubwa yanakuwa dhaifu. Katika kutoa ushauri kwa

wanandoa, nimekutana na zoefu na changamoto mbalimbali zilizo nipelekea kujifunza kuwa Safari ya Ndoa bora na ya kudumu inahitaji maandalizi yaliyo bora na sahihi. Hivyo basi, haya yamekuwa sababu ya kuandika kitabu hiki kwa Vijana wanaojiandaa kwa maisha ya ndoa. Kitabu hiki kitatumika kama njia ya vijana ya kuondokana au kupunguza changamoto za Ndoa huko mbeleni. Naamini kwamba maandalizi ya Ndoa yakifanyika ipasavyo, ***vijana wakipata muda wa kufahamiana vizuri kabla ya kuingia kwenye agano la maisha ya Ndoa,*** changamoto za kwenye Ndoa zitapungua kama siyo kuisha kabisa.

Ni dhahiri kwamba, ***kukosa maandalizi ya ndoa*** ndiko kunasababisha wazazi wengi kushindwa kuishi pamoja kwa amani, wanashindwa kuuvaa utu wema, kushindwa kuishi maisha ya upendo, uvumilivu, unyenyekevu, kushindwa kurekebishana na kuonyana kwa saburi.

Katika kitabu hiki tutaona changamoto mbalimbali za Ndoa za sasa, tutaona visababishi vya changamoto hizo, tutaona ni nini cha kufanya (maandalizi) ili kuepukana na changamoto za ndoa za sasa, ni nini cha kufanya ili kuweza kuishi Ndoa Bora na siyo bora Ndoa.

Ndani ya kitabu hiki, yameelezwa mambo kadha wa kadha kuhusiana na Malezi ya Vijana na Safari ya Ndoa Bora. Ndoa bora ni ipi, ndoa bora inaanzaje, inaanzia wapi, taratibu za ndoa bora ni zipi, Ndoa bora inachukua muda gani kutengenezwa, changamoto za ndoa bora ni zipi, n.k n.k

**Kumbuka;** Ndoa imewekwa na Mungu mwenyewe, Kwa maana hiyo, namna ambavyo Mungu anaheshimiwa, na yote aliyoyafanya pia hayana budi kuheshimiwa. ***"Ndoa Na Iheshimiwe na watu wote, kwanza na wanandoa wenyewe na walio nje ya ndoa hiyo." Waebrania 13:4***

# DIBAJI

**Kuna** methali kongwe ya Kichina inayosema 'Ni bora kuwasha mshumaa kuliko kulalamikia giza'. Ndivyo alivyofanya Mwl. Pancrasia Paul, mwandishi wa kitabu hiki 'Malezi ya Vijana na Safari ya ndoa'. Kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi miaka ya usoni dhidi ya vijana na ubovu wa ndoa. Kumbe Mwl. Pancrasia akaona ni jambo la heri zaidi kuandika kitabu kitakachowasaidia vijana katika changamoto hizo kuliko kulalamika.

Pamoja na kwamba kitabu hiki kina sura saba lakini kwa kweli jina la kitabu chenyewe linapendekeza sura mbili kuu. Sehemu ya kwanza ni **'Malezi ya vijana'** na ya pili ni **'Safari ya ndoa'.**

Katika sehemu ya kwanza mwandishi anagusa moja kwa moja bila longolongo tatizo mama katika malezi ya watoto/vijana kwamba "Waasisi wa familia kushindwa kusimama katika nafasi zao. Waasisi wa familia (Wanandoa) kukosa muda wa kukaa na watoto wao na kuwasikiliza. Waasisi wa familia wanashindwa kufanya kazi yao ya walimu wa kwanza."

Jambo hili ni zito kiasi kwamba mwandishi analiita 'Janga'. Unaposikia kijiji fulani kimepata janga maana yake ni kwamba kilichotokea hapo kimesababisha uharibifu kiasi kwamba wanakijiji wale hawawezi kujiendesha bila msaada kutoka nje. Anachodokeza mwandishi katika nukuu hapo juu ni kwamba baba ameshindwa kuwa baba na mama ameshindwa kuwa mama. Familia sio familia tena. 'Chumvi isiyochumvisha si chumvi hiyo'.

Watoto/vijana wetu wanajiendea kama kondoo bila mchungaji. Wazazi hawana muda wa kuishi na watoto. Kamwe hawapo nyumbani. Hakuna muda wa kuwasikiliza na kuzungumza na vijana.

Sehemu ya pili ya kitabu inaongelea juu ya 'safari ya ndoa'. Mada hii imepewa kipaumbele kwa wingi wa kurasa zilizoandikwa juu yake. Wazo kuu hapa ni kwamba ili kupata ndoa bora walengwa hawana budi kufahamiana vizuri. Kwa uzito wa jambo lenyewe wapendanao wapeane si chini ya miaka miwili ya kusomana na kuchunguzana. Lakini pia kujirekebisha na kurekebishana.

Mwandishi anapigia mstari mawazo matatu ambayo anapambana kwelikweli kuyafafanua.

La kwanza ni kutambua kwamba ndoa ni safari. Safari ya kukutana, kurafikiana, kuongea, kuhojiana n.k. Kwa mtazamo huo, anakemea n**doa za kukurupuka, ndoa za kisanii, ndoa za 'bora ndoa',** ndoa za kwenda likizo **Disemba na kurudi na mke Januari.**

La pili ni juu ya maandalizi bora ya ndoa. Kinachotafutwa hapa ni vijana hawa wawili wafahamiane vya kutosha. Kikwazo kikubwa katika hili ni kukosa ukweli na kuendekeza ngono kabla ya ndoa. Kuna fikra potofu kwamba vijana wakishakutana katika ngono basi tayari wameshafahamiana. Kwa ukali kabisa mwandishi anakataza kwa wapendanao kufanya ngono. Tendo hili pamoja na kuwa ni dhambi pia huzorotesha kabisa mchakato wa kufahamiana. Mwandishi anaamini kabisa, tena kutokana na uzoefu wake binafsi kwamba vijana wakizingatia hili la maandalizi mazuri, wanakuwa na uhakika wa kuwa na ndoa bora. Changamoto hazitakosekana.